TANGAZO LA SERIKALI NA. 779 la tarehe 3/11/2023

SHERIA YA USIMAMIZI WA USHURU WA BIDHAA
(SURA YA 147)

# AMRI

(*Imetolewa chini ya kifungu cha 128*)

AMRI YA MSAMAHA WA USHURU WA BIDHAA KWA MAGARI MANNE YANAYOINGIZWA NCHINI NA FAMILY HEALTH INTERNATIONAL (FH1360) YA MWAKA 2023

Jina na kuanza kutumika

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Ushuru wa Bidhaa kwa Magari Manne Yanayoingizwa Nchini na Family Health International (FH1360) ya Mwaka 2023 na itachukuliwa kuwa ilianza kutumika tarehe 25 Agosti, 2023.

Msamaha

2. Kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika aya ya 3 na masharti mengine yoyote yanayoweza kuainishwa na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, kiasi chote cha ushuru wa bidhaa unaopaswa kulipwa kuhusiana na magari manne yaliyoanishwa katika Jedwali la Amri hii, yanayoingizwa au kununuliwa ndani ya nchi kabla ya kibali cha forodha kwaniaba ya Family Health International (FH1360) kwa ajili ya Mradi wa Msaada wa Kiufundi unasamehewa.

Masharti

3. Msamaha uliotolewa chini ya Amri hii utakoma na ushuru wa bidhaa utapaswa kulipwa kana kwamba Amri hii haikutolewa iwapo magari hayo yatatumika kwa matumizi mengine au yatahamishwa au kuuzwa kwa mtu mwingine ambaye hastahili kupata manufaa yanayotolewa na Amri hii.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

| Na. | Maelezo | Chasis Na. | Injini Na |
|---|---|---|---|
| 1. | Toyota Land Cruiser Hard Top | JTEEB71J70F022621 | 1HZ-1028283 |
| 2. | Toyota Land Cruiser Hard Top | JTEEB71J30F022650 | 1HZ-1028483 |
| 3. | Toyota Land Cruiser Hard Top | JTEEB71J70F022583 | 1HZ-1027986 |
| 4. | Toyota Land Cruiser Hard Top | JTEEB71J70F022601 | 1HZ-1028111 |

Dodoma,
19 Octoba, 2023

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU
*Waziri wa Fedha*